JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

# SHULE YA SEKONDARI GONJA

SIMU :0713 414195
E MAIL: gonjasekondari@gmail.com
WEB: www.gonjasekondari.blogspot.com

S.L.P 679
**GONJA - SAME**
**15 DESEMBA 2021**

---

Kumb Na: **MSS/USAJILI/2021/01**

Kwa mzazi wa …………………………………………………

YAH: **MAAGIZO YA MWANAFUNZI WA KUTWA ANAYEJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GONJA MWAKA 2021**

Ninafuraha kukujulisha kuwa mwanao…………………………………mwenye namba ya mtihani……………………..... amechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Gonja.

Shule itafunguliwa tarehe **11 JANUARI 2019** mwisho wa kuripoti ni tarehe **25 JANUARI 2019.**

MAZINGIRA YA SHULE

Shule ya Sekondari Gonja ni shule ya kutwa ya serikali iliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Shule ipo kwenye kijiji cha Gonja - Mpirani ambapo kuna mazingira mazuri ya kusoma na kujifunzia.

**MICHANGO.**

Michango itatolewa na serikali kwa mujibu wa waraka wa elimu namba 6 wa mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa elimumsingi bila malipo.

Kwa mujibu wa waraka huo pamoja na chakula mzazi atatakiwa kugharamia sare za shule na sare za michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo madaftari na kalamu. Aidha kutakuwa na kikao cha wazazi Jumatano tarehe **30 DESEMBA 2020 saa 4:00 Asubuhi** kwa ajili ya kujadili na kutoa ufafanuzi wa maswala mbalimbali yaliyomo kwenye fomu hii kupanga mikakati ya kitaaluma kabla ya kufungua shule.

**CHAKULA**

Wanafunzi wote wanatakiwa kula shuleni. Hivyo mzazi anatakiwa kuchangia chakula kama ifuatavyo:-

| | **CHAKULA** | **IDADI KWA MUHULA (SIKU 100)** |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi yaliyokobolewa (Makande) | Kg 12.5 |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Mchele | Kg 12.5 |
| 2. | Maharage mazuri yaliyoiva | 12.5 |
| 3. | Mpishi, kuni, chumvi, mafuta n.k. (zitapokelewa na kamati maalumu ya chakula inayosimamiwa na wazazi) | 10,000/= |

*Hatupokei fedha kama mbadala wa chakula. Tafadhali nunua chakula ulete shuleni*

**SARE ZA SHULE:**

| Na | WAVULANA | WASICHANA |
|---|---|---|
| 01 | Mashati mawili meupe yenye kitambaa cha tetron (tomato) yenye kumtosha mwanafunzi yasiyobana(model) yenye mikono mifupi mapya | Blauzi mbili nyeupe zenye kitambaa cha tetron (tomato) zenye kumtosha mwanafunzi zisizobana(model) zenye mikono mifupi mpya.<br><br>HIJABU, atakuwa na hijabu mbili ndefu zisizobana zinazofika kati ya goti na kiuno. Isiyokuwa na mpasuo mkubwa.( fika siku ya kikao kuona mfano wa hijabu inayohitajika) kitambaa kisiwe kinachonesha. |
| 02 | Suruali mbili za rangi ya light blue(blu bahari) na kizibao cha light blue . suruali ziwe pana zisibane. Sare ikiwa tofauti na utaratibu uliowekwa haitapokelewa | Sketi mbili za rangi ya blu bahari(light blue) zisizobana, na vizibao vya rangi ya blu bahari (light blue). Sketi iwe ndefu iliyoshonwa kwa mtindo wa **V**. Kwa maelekezo zaidi fika shuleni. Sare ikiwa tofauti na utaratibu uliowekwa haitapokelewa |
| 03 | Viatu vipya vya ngozi vyeusi lazima viwe na kamba(GIDAMU) jozi mbili | Viatu vipya vya ngozi vyeusi lazima viwe na kamba(GIDAMU) |
| 04 | Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo | Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo |
| 07 | Soksi **NYEUSI** zisizo na picha wala michoro, ziwe ndefu jozi mbili au zaidi | Soksi **NYEUPE** zisizo na picha wala michoro, ziwe ndefu jozi mbili au zaidi |
| 08 | Bukta ya michezo rangi yeyote | Suruali ya traksuti kwa ajili ya michezo yenye rangi ya dark blue(blu nyeusi) |

Sare nyingine ambazo ni muhimu mwanafunzi kuwa nazo ni:-

i. Sweta la rangi ya blu bahari(light blue) (litavaliwa siku za baridi au kama mwanafunzi mgonjwa)

A. VIFAA.

Siku ya kuripoti anatakiwa kuripoti na vifaa vifuatavyo:-

| **NA** | **WANAFUNZI WA KUTWA** |
|---|---|
| 01 | Jembe jipya lenye mpini mzuri |
| 02 | Fyekeo lililonolewa |
| 03 | Vyombo vya chakula ( bakuli, sahani,kijiko na kikombe) kwa ajili ya chakula |
| 04 | Fagio jipya la chelewa la kusimama lenye mpini. |
| 05 | Ndoo moja ndogo mpya ya plastiki yenye mfuniko |

**VIFAA VYA TAALUMA KWA WANAFUNZI**

A) Daftari kubwa kumi na nne(14) counter books sio chini ya 3 quarers
B) Mkebe mmoja
C) Rula moja inayoonesha upande wa pili ya plastic
D) Penseli na kichongeo
E) Begi jipya la kubebea madaftari lisilo na michoro au picha ambazo haziendani na maadili m.f picha zenye jani la mche wa bangi ama mtu anaevuta bangi. Isiwe mfuko wa nailoni(mfuko wa Rambo au marlbolo )
F) Kamusi ya kiingereza kwa kiingereza
G) Vitabu vya kiingereza (MABALA THE FARMER au HAWA THE BUS DRIVER)

1. Ikitokea sare zake zitakuwa hazijakamilika kushonwa mpaka siku ya kufungua shule aje akiwa amevaa sare ya shule alikotoka. Asivae nguo za nyumbani.

2. Mzazi na mwanafunzi anatakiwa kusoma na kuelewa na kusaini fomu ya utii wa mwanafunzi na kuisaini kama kiapo cha nidhamu na utii kwa mwanafunzi awapo shuleni.

ELIMU NI UKOMBOZI!
KARIBU SANA GONJA SEKONDARI

…………………………………………………….
MWL. NYAMBWIRO B.A

MKUU WA SHULE